**OR – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE**
Simu Na: 0738287191/0626701221
E – mail:ruhindasecschool@g.mail.com

SHULE YA SEKONDARI RUHINDA,
S. L.P 571,
**KARAGWE.**

Kumb. Na. RSS/FK/K.1/26 01/12/2024

__________________________________________________

__________________________________________________

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI RUHINDA – 2024.**

Uongozi wa Shule ya Sekondari Ruhinda unayo furaha kukupongeza na kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii kama mwanafunzi wa kutwa/ bweni.

Shule ya Sekondari Ruhinda ni shule mchanganyiko ya wasichana na wavulana inayopokea wanafunzi wa kawaida na wenye mahitaji maalumu. Wanafunzi wa kawaida wanaweza kusoma kutwa au kulala bweni/ hosteli kwa hiari na uwezo wa wazazi wao. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu ni wanafunzi wa bweni moja kwa moja. Usafiri wa kuja shuleni na kwenda likizo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa bweni unagharimiwa na mzazi / mlezi wa mwanafunzi.

## 1. MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari Ruhinda iko Mkoani Kagera, Wilaya ya Karagwe kilometa 22 kutoka makao makuu ya wilaya (Kayanga) na kilometa 15 kutoka mji mdogo uitwao Omurushaka. Unaweza kufika shuleni kwa kupanda mabasi madogo (Hiace) yaendayo Wilayani Ngara kutokaea mjini Bukoba na kushuka Nyaishozi. Kwa wanaotumia magari ya kutoka Mwanza hadi Karagwe katika mji mdogo wa Omurushaka, watatumia magari madogo ya abiria (tax) yanayotokea stendi ndogo ya Bohari na kuteremkia Nyaishozi kisha watachukua usafiri wa pikipiki hadi shuleni Ruhinda.

## 2. MAMBO YA KUZINGATIA

2.1 Shule itafunguliwa tarehe 08/01/2024 siku ya Jumatatu kwa wanafunzi wa kutwa, mwanafunzi atapokelewa kuanzia siku hiyo tarehe hiyo saa 1:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri isipokuwa kwa wanafunzi wa bweni tu.

2.2 Wanafunzi wa bweni wanatakiwa kufika shuleni tarehe 07/01/2023 siku ya Jumapili.

2.3 Mwanafunzi atakayeshindwa kuripoti ndani ya siku 90 atakuwa amepoteza nafasi yake.

## 3. MAHITAJI YA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE WA BWENI NA KUTWA;-

Mwanafunzi anatakiwa afike na mahitaji yafuatayo siku ya kuripoti shule

01. Tsh 6,000 kwa ajili ya bima ya afya.
02. Tsh 4,000 kwa ajili ya tai na nembo.
03. Faili (spring file) dogo kwa ajili ya kumbukumbu za mwanafunzi.

**4. Sare ya Shule .**

**WAVULANA**.

- Suruali mbili zisizobana rangi nyeusi zenye urefu wa kufunika visigino pasipo kuzikanyaga, zenye upana wa ichi 21- 22 miguuni.
  - **Kama rangi ya sare ya shule haitaeleweka njoo shuleni uelekezwe mahali inapopatikana.**
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetroni zenye mfuko mmoja upande wa kushoto zisizobana.
- Mkanda mweusi upana usiozidi inchi 2.
- Jozi ya viatu rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeusi jozi 2.

**WASICHANA**.

- Sketi mbili rangi nyeusi zenye marinda ya kuelekea upande mmoja. Upana wa marinda inchi 2, upana wa mkanda usiozidi inchi 2. Sketi iwe na urefu wa kutosha . Mwanafunzi mwenye sketi fupi hatapokelewa.
  - **Kama rangi ya sare ya shule haitaeleweka njoo shuleni uelekezwe mahali inapopatikana.**
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetroni zenye mfuko mmoja upande wa kushoto zisizobana.
- Jozi ya viatu rangi nyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- Soksi nyeupe jozi 2.

**5. SARE KWA WOTE.**

- Sweta rangi nyekundu iliyokaza (maroon).
- Nywele fupi zisizozidi sentimeta moja. Kusuka, kuweka dawa ya nywele au kunyoa kipara hairuhusiwi. Kubadili rangi ya ngozi na kucha, kuvaa bangili, hereni pete na mkufu pia haviruhusiwi.

- Nguo za michezo: (wavulana bukta na T- shirt za bluu kama za timu ya Chelsea na (wasichana ni suruali na T- shirt nyekundu kama za timu ya Arsenal na viatu vya raba kwa wote).

**6. VIFAA VYA DARASANI.**

- Kalamu za wino na za risasi za kutosha.
- Kasha la vifaa vya hisabati (mathematical instruments set).
- Rula.
- Madaftari ya kutosha makubwa yasiyopungua 12.
- Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza (English – English Dictionary).
- Rimu 01 ya karatasi kwa ajili ya mitihani na mazoezi.

**7. VIFAA VYA NJE/ KUJITEGEMEA NA USAFI.**

- Ndoo 1 ya plastiki ya lita 20 kwa ajili ya kuchotea maji ya chakula – wanafunzi wote.
- Mfagio wa nje (chelewa) – wanafunzi wote.
- Mfagio wa ndani (soft broom) – wanafunzi wote.
- Mopa - wanafunzi wote.
- Jembe na mpini (wavulana).
- Kotama (wasichana).

8. **MAHITAJI YA USAJILI (WOTE).**

- Fomu iliyojazwa na daktari kuthibitisha afya ya mtoto (KIAMBATISHO ‘A’)
- Cheti cha kuzaliwa.
- Fomu za utambulisho (zimeambatanishwa – kiambatisho B na C), zijazwe kwa ukamilifu na ziwasilishwe shuleni wakati wa kuripoti.
- Sheria za shule: utatakiwa kusoma sheria za shule (kiambatisho D) na kusaini kukubali kuzifuata.

**9. MAHITAJI YA WANAFUNZI WA BWENI (WENYE MAHITAJI MAALUMU)**

- Godoro dogo inchi $2^1/_2$
- Magauni mawili ya kushindia marefu rangi ya bluu.
- Track suit ya kijivu kwa ajili ya kushindia.
- Pedi zisizopungua pakti 6 (wasichana).
- Mashuka jozi mbili rangi ya bluu bahari.
- Blanketi 1.
- Mto na foronya za rangi ya bluu bahari.
- Chandarua 1 (rangi ya bluu bahari).
- Sanduku kubwa la chuma/mbao lenye kufuri imara.
- Kandambili za kuogea.
- Vifaa vya kulia chakula – sahani na kikombe (vya mfupa) pamoja na kijiko.
- Pea moja ya kitenge au kanga kwa ajili ya kuogea(wasichana).
- Taulo ya kuogea .
- Jarabibi nyeusi kwa ajili ya kushindia (wanafunzi waislam).
- Nguo za ndani za kutosha na hasa kwa wasichana .
- Mswaki na dawa ya meno.
- Sabuni za kufulia na za kuogea za kutosha .
- Dawa ya viatu na brashi.
- Sweta yenye rangi ya bluu kwa ajili ya kushindia.

N.B: Hairuhusiwi kabisa kuja na nguo au vifaa tofauti na vilivyotajwa hapo juu mfano makoti, majaketi n.k atakayekuja navyo shule itavitunza na mwanafunzi atakabidhiwa vifaa hivyo atakapohitimu kidato cha nne.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI RUHINDA**

…………………………..
**AMBRUCE ABEL KATOROGO**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI UHINDA**

**KIAMBATISHO A**
**KARAGWE DISTRICT COUNCIL**
**RUHINDA SECONDARY SCHOOL**

**STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION REPORT**

1. STUDENT'S NAME …………………………………………………………………………
2. AGE ……………….. HEIGHT (CM) ………………… WEIGHT (KG) …………………..
3. BLOOD EXAMINATION: HAEMOGLOBIN ……………………………………………..…
   BLOOD GROUP ……………………………………………....
4. ANY ABNORMALITIES OBSERVED ……………………………………………………..
5. STOOL EXAMINATION …………………………………………………………………………
6. URINALYSIS ……………………………………………………………………………………
7. TB TEST (If negative, was immunization given?) ……………………………………………...
8. CHEST …………………………………………………………………………………………..
9. ANY COMPLAINT NOTED IN RELATION TO:
   a) ASTHMA ……………………………………………………………………………
   b) HEADACHE ……………………………………………………………………………
   c) INABILITY OF CERTAIN FOOD (MENTION THE REASON BEHIND) ……………………………………………………………………………………………
   d) SKIN DISEASES ……………………………………………………………………….
   e) BILHARZIA (to be observed in distinguished clinics)…………………………………

10. IS THERE ANY THING ELSE TO BE KNOWN BY THE SCHOOL ADMINISTRATION? ....................................................................................................…………………………….
11. ANY TREATMENT GIVEN ……………………………………………………………………
12. DOCTOR'S / MEDICAL OFFICE'S RECOMMENDATIONS:
…………………………………………………………………………………………………......

N.B: IN CASE ANY OF THE ABOVE REQUESTED EXAMINATION IS NOT UNDER GONE OR CARRIED OUT, DO NOT DO ANYA DAMARCATION OR WRITE ANYTHING FOR THE SAKE OF FUTURE CONVENIENCE.

13. DATE ……………………………… SIGNATURE OF EXAMINE ………………………
DESIGNATION
………………………………………………..
STATION
………………………………………………….
OFFICIAL STAMP

**KIAMBATISHO 'B'**

**FOMU HII IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI.**

Shule ya Sekondari Ruhinda,
S. L. P 571,
KARAGWE.

**MAHUSIANO NA MZAZI / MLEZI**

1. Wazazi / mlezi wanajulishwa kuwa barua yenye kuleta ujumbe muhimu kwa mwanafunzi kama kumwombea ruhusa, au kuja nyumbani kwa shughuli muhimu/ maalum ni lazima iandikwe na kusainiwa na mzazi/mlezi aliyeandikishwa na anayetambulika shuleni.

2. Kuhusu masuala mbalimbali yanayomhusu mwanafunzi, shule haitakuwa tayari kuyajadili na mtu/ndugu anayejitokeza. Bali masuala yote yamhusuyo mwanafunzi yatajadiliwa au mawasiliano yatafanyika kati ya shule na mzazi/ mlezi aliyeandikishwa shuleni tu. Wengine hawatakubalika labda kwa idhini maalumu itakayoandikwa na kusainiwa na mzazi/ mlezi mwenyewe.

**(WAHUSIKA NI HAWA PEKEE)**

1. Jina la Baba ……………………………………………………….. (hai/ marehemu)
   Kazi (kama hai) ……………………………………………………………
   ANWANI: ………………………………………………………………...
   Simu Na……………………………………………………………………

2. Jina la Mama ……………………………………………… (hai/ marehemu)
   Kazi (kama ni hai) ………………………………………………………….
   ANWANI: ………………………………………………………………………………..
   Simu Na ………………………………………………………………..

***Mlezi ni Yule uliyemteua kukuwakilisha katika masuala yanayohusu mwanafunzi huyu****

3. Jina la mlezi …………………………………… Uhusiano …………………
   ANWANI ……………………………………… Simu Na………………
   JINA NA SAHIHI YA MZAZI ALIYEMTEUA MLEZI …………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   TAREHE …………………………………………

**N.B: (JAZA SEHEMU ZOTE TATU KWA WATU WATATU TOFAUTI)**

**KIAMBATISHO C**

**SHULE YA SEKONDARI RUHINDA**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI (**Yajazwe na mwanafunzi mwenyewe)

01. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI …………………………………………………………..
    (Jaza kama ilivyo kwenye TSM 9)
02. ANUANI YA NYUMBANI: …………………………………………………………
    TAREHE YA KUZALIWA: ………………………………………………………………
03. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI;-
    MAHALI ULIPOZALIWA:
    A. JINA LA WILAYA …………………………………. TARAFA …………………….
       KATA: …………………………………………… KIJIJI …………………………….
       KITONGOJI ………………………………………………….
    B. SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA ………………………………………………..
       ANUANI …………………………………………………..
    C. DINI YAKO ………………………………………………. TAIFA *MTANZANIA/SI MTANZANIA (Futa lisilo sahihi)
04. JAMAA KATIKA FAMILIA YAKO
    A) JINA LA BABA ………………………………………………………………
       ANUANI …………………………………NAMBA YA SIMU ……………………........
       ANAISHI/ HAISHI
       KAZI YAKE …………………………………………………………………..
    B) JINA LA MAMA …………………………………………………………………
       ANUANI……………………………….. NAMBA YA SIMU ………………………..
       ANAISHI/ HAISHI
       KAZI YAKE ……………………………………………………………………

    C) JINA LA MLEZI ……………………………………………………………………
       ANUANI ……………………………….. NAMBA YA SIMU ………………………..
       ANAISHI/ HAISHI
       KAZI YAKE ……………………………………………………………………..
       UHUSIANO WA MLEZI NA WEWE
    D) IDADI YA KAKA ZAKO ……………………………………………………………
    E) IDADI YA DADA ZAKO ……………………………………………………………..
    F) WEWE NI MTOTO WA NGAPI KATIKA FAMILIA? ………………………………

Mimi ………………………………………………. (mzazi/ mlezi) wa mwanafunzi) ………………………………………….. nimehakikisha kuwa taarifa zilizotajwa hapo juu ni za kweli.

JINA LA MZAZI/ MLEZI …………………………………………………………

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI ……………………………………………………….

**KIAMBISHO 'D'**
**SHULE YA SEKONDARI RUHINDA**
**SHERIA ZA SHULE.**

**A HESHIMA.**

i. Unatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
ii. Hairuhusiwi kwa wanafunzi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
iii. Kila mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
iv. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kufanya mambo yafuatayo;-
    a) Kuvuta sigara.
    b) Kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu zisizowekwa katika hali ya usafi.
    c) Kufuga ndevu.
    d) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.
    e) Kugombana.
v. Mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja na kukimbia aliko mwalimu au mfanyakazi wa shule aliyemwita.
vi. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
vii. Wanafunzi watasimama katika mistari kupokea huduma yoyote.
viii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mfano bora kwa heshima na tabia njema mahali popote atakapo kuwa .
ix. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kutunza darasa, ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali zote za Umma.
x. Kila mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu swali.
xi. Kila mwanafunzi anatakiwa kutopiga kelele wakati wote anapokuwa darasani, bwenini au katika mazingira ya shule na asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
xii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizoko katika jamii na kuzoea kuishi katika jamii yenye tofauti hizo.
xiii. Kila mwanafunzi anatakiwa kuongea lugha ya kufundishia ambayo ni kiingereza muda wote.

**B MAHUDHURIO.**

i Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni kwa muda wote wa masomo.
ii Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
iii Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule, kama vile baraza la shule, vikao vya madarasa, vikao vya bwenini n.k.
iv Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria paredi, kukaguliwa usafi kupandisha Bendera ya Taifa na kuimba nyimbo za Tanzania na uzalendo.

**C KUWAHI.**

i Kila mwanafunzi anapaswa kuthamini muda na kuutumia vizuri anapofanya shughuli zote za shule na kuzikamilisha kwa muda uliopangwa.
ii Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa na kufanya kazi zote anazopewa na mwalimu au mfanyakazi wa shule.
iii Kila mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa na kuwahi shuleni asubuhi kwa muda uliopangwa.

**D SARE YA SHULE.**

i. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote wa;-
   a) Masomo darasani.
   b) Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
   c) Baraza la shule.
   d) Kwenda hospitalini.
   e) Maandamano.
   f) Kusafiri kuja shuleni au kwenda kwao wakati wa likizo.

ii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nguo za michezo na kuzitumia wakati wa michezo tu.

iii. Kofia, viatu vya ghorofa, pamoja na mapambo mengine hayaruhusiwi kuvaliwa pamoja na sare ya shule

iv. Sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa shuleni yanatakiwa kuwa safi muda wote.

v. Mwanafunzi lazima awe na kitambulisho cha shule anaposafiri nje ya shule au likizo.

**E MIPAKA YA SHULE.**

i Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutoka nje ya shule bila kibali maalum.

ii Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutembea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali / ruhusa maalum:
   a) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
   b) Ofisi za shule.
   c) Maabara.
   d) Jikoni.
   e) Stoo za shule.

iii Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo:
   a) Vilabu vya pombe.
   b) Majumba ya starehe.
   c) Majumba ye kufikia wageni (Guest House).

**F USAFI.**

Ni lazima kwa mwanafunzi kutunza usafi wa mwili wake na mazingira, na hali hii ichukuliwe kama sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku.

**G MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA.**

i Wizi.
ii Uasherati, ubakaji na ushoga.
iii Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
iv Uvutaji bangi.
v Makosa mengine yote ya jinai.
vi Kupigana au kupiga.
vii Kuharibu makusudi mali ya Umma.
viii Kuharibu Bendera ya Taifa.
ix Kuoa au kuolewa.
x Kupata au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
xi Kutoa mimba.
xii Kugoma, kuchochea na koungoza migomo au kuvuruga amani.
xiii Kukataa adhabu kwa makusudi.
xiv Kumiliki simu ya mkononi.

**H AHADI YA MWANAFUNZI.**

Mimi …………………………………………………………… nimesoma sheria zote za shule na kuzielewa na nitazitekeleza ipasavyo.

Jina la mwanafunzi …………………………………… sahihi ………………….